

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA NISHATI NA MADINI**



**TAARIFA KWA UMMA**

**ZUIO LA USAFIRISHAJI WA MAKINIKIA (*CONCENTRATES*) NA  
MAWE YENYE MADINI (*ORE*) KWENDA NJE YA NCHI**

Wizara ya Nishati na Madini inapenda kuujulisha Umma, Kampuni na watu wanaojihusisha na uvunaji wa madini nchini, kuwa usafirishaji wa makinikia (*concentrates*) na mawe yeye madini (*ore*) ya *metallic minerals* kama vile dhahabu, shaba, nikeli na fedha umesitishwa kuanzia tarehe 02 Machi, 2017. Usitishwaji huu unalenga kuhakikisha kuwa madini yanayochimbwa hapa nchini yanaongezewa thamani kabla ya kusafirishwa kwenda nje hasa kwa ajili ya uyeyushaji (*smelting*) na usafishaji (*refining*) ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na Sheria ya Madini ya Mwaka 2010. Aidha, shughuli za uongezaji thamani madini hapa nchini zitatoa fursa ya ajira, mapato na kuhawilisha teknolojia na hivyo kuleta manufaa zaidi kwa Taifa.

Hivyo, ni mategemeo yetu kuwa Kampuni na watu wote wanaovuna madini nchini ambao walikuwa wanasafirisha makinikia ya madini pamoja na mawe yenye madini watazingatia ipasavyo kutosafirisha tena kwenda nje ya nchi kwa ajili ya uyeyusahji na usafishaji. Wanatakiwa kuanza taratibu za kufanya shughuli hizo hapa nchini. Serikali itatoa ushirikiano unaotakiwa kwa Kampuni au watu watakaojishughulisha na shughuli za uchenjuaji madini hapa nchini hasa uyeyushaji na usafishaji wa madini.

Imetolewa na ;

**KATIBU MKUU  
WIZARA YA NISHATI NA MADINI  
3 Machi, 2017**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
MINISTRY OF ENERGY AND MINERALS**



**PRESS RELEASE**

**EXPORT BAN OF METALLIC MINERAL CONCENTRATES AND  
ORE**

The Ministry of Energy and Minerals would like to inform the public, companies and individuals involved in minerals extraction that export of mineral concentrates and ores for metallic minerals such as gold, copper, nickel and silver has been banned with effect from 2<sup>nd</sup> March, 2017. The ban intends to make sure that mineral value addition activities are carried out within Tanzania as emphasized in the Mineral Policy of 2009 and Mining Act of 2010. Mineral value addition activities will provide employment opportunities, revenues and technology transfer, hence more benefits to the nation.

Therefore, it is expected that all the companies and individuals who were exporting concentrates and mineral ores to foreign countries for beneficiation (processing, smelting or refining) will immediately stop and start doing such activities within the country. The Government will provide any necessary support to stakeholders involved in mineral beneficiation activities within the country, particularly smelting and refining of minerals.

Issued by;

**PERMANENT SECRETARY  
MINISTRY OF ENERGY AND MINERALS  
March 03, 2017**